

Asante kwa kupata chanjo ya COVID-19 ili kukufanya wewe, familia yako, na jamii yako kuwa wenyе afya na salama.



Inachukuliwa kuwa una kinga, au kulindwa kutokana na virusi, wiki 2 baada ya kupokea dozi yako ya mwisho ya chanjo ya COVID-19. Hata hivyo, ikiwa umekuwa katika hatari ya kuambukizwa virusi kabla ya kupata dozi yako ya mwisho ya chanjo, au ulikuwa katika hatari kabla ya mwili wako kutengeneza kinga kamili, bado unaweza kuugua.




Unapaswa bado kuendelea kucaa barakoa na kuchukua tahadhari ili kuzuia kuenea kwa COVID-19 hadi watu wengi zaidi waweze kupata chanjo.

Chanjo zote za COVID-19 zilizoidhinishwa na FDA ni salama na zinfaa katika kukukinga dhidi ya virusi hivyo. Zinakukinga usiugue, kulazimika ulazwe hospitalini au kufariki kutokana na COVID-19. Chunguzi za hivi karibuni¹ zinaonyesha chanjo zinaweza kuzuia maambukizi ya virusi kwa watu wengine na kukabiliana na aina mpya tofauti za virusi zilizotambuliwa hadi sasa.

Hadi wataalam wa matibabu watakobaini katika hali halisi ya maisha ikiwa bado unaweza kusambaza virusi kwa wengine baada ya kupata chanjo au la, ni muhimu kuendelea kutumia zana zote zinazopatikana kwetu ili kusaidia kumaliza janga hili: vaa barakoa wakati wowote unapokuwa karibu na watu ambao hawaishi nyumbani kwako, kaa futi 6 (mita 2) mbali na watu wengine, nawa mikono yako mara kwa mara, na ukae nyumbani unapoumwa. **Mara tu watu walio wengi zaidi watakopokuwa wamepata chanjo, maisha yanaweza kuanza kurejea katika hali ya kawaida.**

Aina tofauti za COVID-19

Aina tofauti za baadaye za COVID-19 (wakati mwengine huitwa uzao) zinaweza kuwa na uwezo wa kuambukiza zaidi ikilinganishwa na aina za hapo awali za COVID-19. Kwa hivyo sasa inahimizwa zaidi, wakazi wa Utah wavae barakoa, wadumishe kutotangamana, na waepuke mikusanyiko mikubwa.



¹ <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/science/science-briefs/fully-vaccinated-people.html>

Je, chanjo za COVID-19 zinaathiri viyi miongozo ya karantini na kujitenga?

Endapo imepita zaidi ya wiki 2 tangu upate dozi yako ya mwisho ya chanjo, sio lazima ujiweke karantini, hata ikiwa umetangamana kwa karibu na mtu aliye na maambukizi. Hata hivyo, kuna mazingira fulani ambapo unaweza kuhitaji kujiweka karantini au kujitenga, hata baada ya kupata chanjo ya COVID-19.

Nini cha kufanya ikiwa una dalili za COVID-19:

Ikiwa una dalili za COVID-19 na:	
Bado hujapata chanjo	Hujapata chanjo kamili (umepata dozi 1 tu kwa chanjo ya dozi 2, kama vile Pfizer au Moderna)
<u>Jitenge</u> na upimwe mara moja.	<u>Jitenge</u> na upimwe mara moja.

Ikiwa umepata chanjo kamili na una dalili za COVID-19:

(umepata dozi 2 kwa chanjo ya Pfizer au Moderna au dozi 1 kwa chanjo ya Johnson & Johnson)

Kama wiki 2 HAZIJA KAMILIKA tangu upate chanjo	Ikiwa angalau wiki 2 zimepita tangu upate chanjo
<u>Jitenge</u> na upimwe mara moja.	Jitenge na mpigie simu daktari au mtoe huduma wako wa afya. Kuna uwezekano kwamba kitu kingine mbali na COVID-19 kinasababisha dalili zako. Hata hivyo, huenda daktari wako akataka upimwe COVID-19. Chanjo za COVID-19 haziathiri usahihi wa kipimo.

Nini cha kufanya ikiwa utatangamana kwa karibu na mtu aliye na maambukizi:

Endapo hujapata dozi yako ya mwisho ya chanjo na umetangamana kwa karibu na mtu aliye na maambukizi:	
Bado hujapata chanjo	Hujapata chanjo kamili (umepata dozi 1 tu kwa chanjo ya dozi 2, kama vile Pfizer au Moderna)
<u>Jiweke karantini</u> na upimwe COVID-19.	<u>Jiweke karantini</u> na upimwe COVID-19.

Ikiwa umepata dozi **yako ya mwisho** ya chanjo na umetangamana kwa karibu na mtu aliye na maambukizi:

(umepata dozi 2 kwa chanjo ya Pfizer au Moderna au dozi 1 kwa chanjo ya Johnson & Johnson)

Kama wiki 2 HAZIJA KAMILIKA tangu upate chanjo	Ikiwa angalau wiki 2 zimepita tangu upate chanjo
<u>Jiweke karantini</u> na upimwe COVID-19.	Huhitaji kujiweka karantini. Hata hivyo, ikiwa utaonyesha kuwa na dalili za COVID-19 baada ya kutangamana kwa karibu na mtu aliye na maambukizi (hali ambayo ni nadra), piga simu kwa daktari au mtoe huduma wako wa afya. Huenda ukahitaji kupimwa COVID-19.